# IDARA YA KAZI YA MAINE

*Kitengo cha Urekebishaji wa Kitaalamu*

Mshirika mwenye kujivunia wa mtandao wa americanjobcenter®







# KIJITABU CHA MAELEKEZO CHA WATUMIAJI

## kwa Huduma za Urekebishaji wa Kitaalamu

**Desemba 2020**

VR100
URKEBISHAJI WA KITAALAMU • 1920-2020


*Kitengo cha Urekebishaji wa Kitaalamu*
*Ofisi ya Huduma za Urekebishaji*


*Imeundwa kwa kushirikiana na*
*Baraza la Urekebishaji la Jimbo la Maine*

**Fahirisi**


Utangulizi ..... 1
Je, nitastahiki huduma za DVR? ..... 2
Ustahiki kwa Wanafunzi wa Mpito ..... 2
Uchaguzi wa Mtumiaji Aliyearifiwa ..... 3
Je, ninawezaje kuunda Mpango wa Ajira Unaomlenga Mtu Binafsi ulio wa ufanisi na umuhimu? ..... 4
Mpango wa Ajira Unaomlenga Mtu Binafsi ni nini? ..... 4
Kuandaa mpango wa kufikia lengo ..... 5
Mambo ambayo DVR inahitaji kuangalia kabla ya kukubaliana na IPE yako ..... 6
Je, nifanye nini ikiwa ninataka kubadilisha IPE yangu AU ikiwa ninahitaji huduma zaidi? ..... 6
Ni nani atakayelipia huduma ninazohitaji? ..... 7
Utakapofikia lengo lako la ajira ..... 8
Huduma ambazo DVR inaweza kutoa ..... 8
Nini kitatokea kwa manufaa yangu ikiwa nitaenda kazini? ..... 9
Ninawezaje kupata taarifa ambayo ninahitaji kuhusu manufaa ili niweze kufanya uchaguzi mzuri wa kitaalamu? ..... 9
Nifanye nini ikiwa sikubaliani na DVR? ..... 10
Wasiliana na Mpango ya Msaada wa Wateja (CAP - Client Assistance Program ) ..... 10
Taratibu za Utatuzi wa Migogoro ..... 2
Huduma za DVR ..... 3
Uzoefu wa Kazi ya Kulipwa ..... 3
Mafunzo ya Kazi na Ajira Zingine Zinazopatikana ..... 5
Mafunzo ya kazi ni nini? ..... 5
Ajira Inayosaidiwa ..... 5
Wakati lengo lako la ajira linahitaji Mafunzo ..... 5
Mafunzo ya Ajira ni nini ..... 5
Je, DVR inaweza kusaidia na mafunzo ya ajira? ..... 5
Ni nini kinachotarajiwa kutoka kwangu ikiwa DVR itanisaidia katika elimu ya juu? ..... 6
Huduma za Kujiajiri ..... 6
Mara tu biashara ndogo inapoanza kufanya kazi: ..... 7
Huduma za Vijana za DVR ..... 8
Mipango ya mpito kutoka shule kwenda kazini ..... 8
Huduma za Mpito za Kabla ya Ajira ..... 8
Huduma Zipi Zinazotolewa na VR ..... 8
Ajira Inayoendelea ..... 9
Teknolojia ya Urekebishaji/ Teknolojia Saidizi ..... 10
Je, ni mchakato gani wa kupata huduma za teknolojia ya urekebishaji? ..... 10
Programu ya Mkopo wa Vifaa vya Adaptive (AELP) ..... 11
Huduma zingine zinazopatikana kutoka kwa Urekebishaji wa Kitaalamu ..... 12

Idara ya Viziwi, Wenye Matatizo ya Kusikia, na Waliopoteza Uwezo wa Kusikia Baadaye (Division for the Deaf, Hard of Hearing, and Late Deafened) ... 12
Huduma za Maisha ya Kujitegemea ... 12
Mpango wa Huduma za Maisha ya Kujitegemea ni nini? ... 12
Rasilimali ... 2
Ninawezaje kufanya uchaguzi mzuri wa kazi? ... 2
Urekebishaji wa Kitaalamu, Elimu ya baada ya Sekondari, Mafunzo na wewe: Mwongozo wa Mtumiaji ... 3
Ofisi za Idara ya Urekebishaji wa Kitaalamu ... 6

## Utangulizi

Kijitabu hiki cha maelekezo kimeundwa kutoa taarifa za jumla kuhusu mpango wa Urekebishaji wa Kitaalamu unaotolewa kupitia Idara ya Kazi ya Maine, Ofisi ya Huduma za Urekebishaji, Idara ya Urekebishaji wa Kitaalamu (DVR - Division of Vocational Rehabilitation). Kusudi ni kukusaidia kuelewa mpango huu na kufanya uwe bora kwako.

Mpango wa Urekebishaji wa Kitaalamu wa Umma ni matokeo ya sheria ya serikali ya kitaifa, Sheria ya Urekebishaji kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Ubunifu na Fursa ya Kazi. Sheria hii inatokana na imani kwamba watu wote wenye ulemavu wanaweza kufanya kazi. Chini ya sheria hii, kila jimbo linaendesha mpango kwa kushirikiana na serikali ya kitaifa. Gharama pia zinagawanywa kati ya serikali ya jimbo na serikali ya kitaifa. Lengo la mpango huu ni kusaidia watu wenye ulemavu (vijana na watu wazima) kujiandaa, kupata, kuendeleza na kudumisha ajira nzuri.
Kushirikisha waajiri ni kipengele muhimu cha mpango wa VR. Wanachama wa timu ya Urekebishaji wa Kitaalamu wanahusika katika kufanya jitihada ya ufikiaji wa biashara ili kutambua mahitaji ya wafanyikazi wote ambayo husababisha kuziba pengo kati ya mahitaji ya waajiri na kuwaweka watafutaji kazi wenye ulemavu. Zaidi ya hayo, kushirikiana na waajiri husababisha kuongezeka kwa ushirikiano na fursa kwa vijana walioko katika mpito kuchunguza nyanja mbalimbali kupitia mahojiano ya habari, ziara za kazi na fursa zingine za kujifunza kazi.

Ajira ni sehemu muhimu katika kusaidia maisha kamili na jumuishi katika jamii yako. Hapa DVR tunaamini kwamba kila mtu yuko tayari kwa kitu, kila mtu yuko tayari kuchukua hatua kwenye njia ya kupata ajira.

Kabla ya kufanya uamuzi wa kutuma maombi unaweza kutaka kutembelea Tovuti ya DVR. Tovuti inajumuisha taarifa kuhusu mpango wa VR ikiwa ni pamoja na huduma za mpito, rasilimali na huduma za ziada za Idara ya Kazi. Kutuma maombi ya VR tafadhali tembelea tovuti ya Maine Kutuma maombi ya DVR kwa toleo la mtandaoni au la kuchapishwa.

IDARA
YA KAZI
YA MAINE
*Kitengo cha Urekebishaji wa Kitaalamu*
Mshirika mwenye kujivunia wa mtandao wa
americanjobcenter®

*Jimbo la Maine hutoa fursa sawa katika ajira na mipango. Vyombo vya usaidizi na huduma za ziada zinapatikana kwa watu wenye ulemavu zinapoombwa.*
*Piga simu kupitia 207-623-6799. Watumiaji wa TTY wapiga simu kwa Mtambo wa kupokea na kurushia habari wa Maine Relay 711.*

## Je, nitastahiki huduma za DVR?

Mara unapofanya uamuzi wa kutuma maombi ya huduma kwa Idara ya Urekebishaji wa Kitaalamu (DVR), hatua inayofuata ni kufanya kazi kwa karibu na Mshauri wako wa VR ili kubaini ustahiki wako. Mara tu maombi yako yatakapopokelewa, utawasilianwa nawe ili kupanga kikao cha kwanza. Taarifa hukusanywa kutoka kwako katika kikao hiki kuhusu jinsi ulemavu wako unavyoathiri uwezo wako wa kufanya kazi, na ikiwa unahitaji huduma za urekebishaji wa kitaalamu ili kupata, kudumisha, au kuendeleza ajira.

Lengo letu ni kufanya uamuzi wa ustahiki wako haraka iwezekanavyo na tukifanya vipimo na kujaza hati chache zaidi. Sheria inahitaji mchakato huu ukamilike kwa muda usiozidi siku 60. Ikiwa kuna haja ya kuzidi siku 60, nyongeza maalum ya muda itakubaliwa kati yako na Mshauri wako wa VR.

Uamuzi wa ustahiki unaweza kuwa wa haraka ikiwa unapokea Bima ya Ulemavu ya Usalama wa Jamii (SSDI - Social Security Disability Insurance) au Mapato ya Ziada ya Usalama (SSI - Supplemental Security Income) na unapanga kufanya kazi.

Mbali na ustahiki wa msingi, DVR kwa sasa ina sera ambayo inatoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu mkubwa zaidi. Hii inaitwa Mpangilio wa Uteuzi (Order of Selection). Mpangilio wa Uteuzi ni muhimu wakati mahitaji ya huduma yanazidi rasilimali za shirika.

Wakati mwingine inaweza kuwa muhimu kwa DVR kupanga vipimo vya matibabu au tathmini zinginezo ili kuamua ustahiki wako au kipaumbele chini ya Mpangilio wa Uteuzi. Hii itafanyika bila gharama yoyote kwako. Unahimizwa kushiriki katika jinsi tathmini hizi zinavyofanywa, ikiwa ni pamoja na uteuzi wa watoa huduma wa kufanya tathmini hizi.

Mifano ya baadhi ya aina za tathmini za DVR ni pamoja na:

- Kukusanya taarifa kuhusu historia yako na rekodi zozote zinazothibitisha ulemavu wako
- Uzoefu wa kazi ya majaribio
- Tathmini ya kisaikolojia
- Tathmini ya matibabu
- Kuzungumza na wewe ili kubaini jinsi ulemavu wako unaweza kuathiri ajira
- Tathmini zingine ambazo zimeamuliwa kuwa muhimu na wewe na Mshauri wako wa VR

Mara tu unapopatikana kuwa unastahiki, hatua inayofuata ni kuandaa Mpango wa Ajira Unaolenga Mtu Binafsi (IPE - Individualized Plan for Employment).

| Vidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| *Bofya hapa kutazama Kanuni za DVR kuhusu mpango wa VR |
| *Tembelea tovuti ya DVR ili kutazama fomu ya maombi au kukamilisha kutuma maombi mtandaoni |
| *Uliza ikiwa unapaswa kuleta kitu chochote kwenye miadi yako. Ikiwezekana, pata rekodi za matibabu au elimu ambazo DVR itahitaji. |

### Ustahiki kwa Wanafunzi wa Mpito

- Wanafunzi wenye umri wa miaka 14-21, wanaopokea huduma kupitia IEP au Mpango wa Sehemu ya 504
- Wana ulemavu uliothibitishwa ambao unawazuia kupata au kudumisha kazi; au
- Wanahitaji huduma za VR kupata au kudumisha kazi. Shule ya sekondari na rekodi za matibabu zinaweza kutoa hati muhimu za uthibitisho zinazohitajika.
- Kamilisha Fomu ya usajili wa Mpito wa Kabla ya Ajira Au fomu ya maombi ya VR

Wanafunzi wanaweza kuwa wanastahiki huduma za urekebishaji wa kitaalamu au "wanaoweza kustahiki".
Wanafunzi ambao "wanaweza kustahiki" ni pamoja na wale ambao wamesajiliwa na VR lakini ambao hawajawasilisha maombi kwa VR. Wanafunzi "wanaoweza kustahiki" wanaweza kupokea Huduma za Mpito za Kabla ya Ajira.

Ikiwa mwanafunzi anapata Bima ya Ulemavu ya Usalama wa Jamii (SSDI) au Mapato ya Ziada ya Usalama (SSI) kulingana na ulemavu wake na ana nia ya kufanya kazi, mwanafunzi huyo anachukuliwa kuwa anastahiki.

Tafadhali angalia Sehemu ya Mpito ya DVR kwenye ukurasa wa 17 kwa taarifa zaidi.

| Vidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| *Kuna Washauri wa VR katika kila shule ya sekondari katika Jimbo lote. Kwa kuongezea, Washauri wa VR hufanya kazi na vijana ambao wanasomea nyumbani au kuhudhuria taasisi zingine za elimu |
| *Kama una maswali yoyote, wasiliana na ofisi ya eneo lako kuuliza kuhusu ni hati unazofaa kukamilisha |

## Uchaguzi wa Mtumiaji Aliyearifiwa

Uchaguzi wa Mtumiaji Aliyearifiwa ni dhana ambayo inapaswa kuongoza maamuzi yote ambayo yanafanyika katika uzoefu wako na Urekebishaji wa Kitaalamu (VR). Sheria ya Urekebishaji inasema kuwa wewe ni mshirika sawa katika maamuzi yote yanayohusu:

- Tathmini yako
- Malengo yako ya ajira
- Huduma za Urekebishaji wa Kitaalamu
- Uchaguzi wa watoa huduma
- Njia za kupata huduma za Urekebishaji wa Kitaalamu

Uchaguzi zilizoarifiwa pia unamaanisha kuwa umefahamishwa kuhusu taarifa na chaguzi zote zinazopatikana. Ikiwa unahitaji usaidizi kuelewa chaguzi hizi au msaada katika kutekeleza kazi hizi, unaweza kuuliza Mshauri wako wa VR, mtu unayemjua, au mtetezi kutoka kwa Mpango wa Msaada wa Mteja (CAP).

Ni muhimu kwako kufanya kazi pamoja na Mshauri wako wa VR na wengine ambao wanakusaidia kufikia lengo lako la ajira. Kuna mambo yanayoathiri chaguzi kama vile: uwezo na vipawa vyako, soko la kazi, masuala ya kisheria na usalama, gharama nafuu, rasilimali za kifedha zinazopatikana, nk. Kwa hivyo, ni muhimu sana kwako na Mshauri wako wa VR kuchunguza njia za kazi ambazo zitapelekea matokeo ya ajira yenye maana.

Uchaguzi wa Mtumiaji Aliyearifiwa ndio msingi wa uzoefu wako na VR. Jadili ushirikiano huu mara nyingi na Mshauri wako wa VR.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| *Ni muhimu kwako kushiriki katika nyanja zote za kufanya maamuzi |
| *Fikiria kuhusu maslahi yako ya ajira kabla ya kukutana na Mshauri wako wa VR. Fikiria kwa uangalifu kuhusu kile unachopenda, chukia, uwezo na mahitaji yako. Kuwa na mawazo ya kujadili na Mshauri wako wa VR inaweza kuwasaidia kujuana |

## Je, ninawezaje kuunda Mpango wa Ajira Unaomlenga Mtu Binafsi ulio wa ufanisi na umuhimu?

### Mpango wa Ajira Unaomlenga Mtu Binafsi ni nini?

Mpango wa Ajira Unaomlenga Mtu Binafsi (IPE - Individualized Plan for Employment) ni hati iliyoandikwa na wewe na Mshauri wako wa VR (VRC) ambayo inaelezea lengo lako halisi na mpango wa jinsi utakavyofikia lengo hilo. Ni matokeo ya kuchambua mambo kama vile soko la kazi la eneo lako, uzoefu wako wa kazi wa awali, njia za kazi, jinsi ulemavu wako unavyoathiri uwezo wako wa kufanya kazi na aina ya kazi ambayo unapendezwa nayo. Mpango huu unaelezea jinsi utakavyopata ajira kwa msaada wa huduma za urekebishaji wa kitaalamu. IPE itaundwa ndani ya siku 90 baada ya kuthibitishwa kuwa unastahiki huduma. IPE huundwa kulingana na Tathmini ya Kina ya Mahitaji ya Urekebishaji, ambayo inategemea taarifa ambayo umeshiriki na VRC wako na taarifa zilizopatikana kupitia mipango ya kitaaluma. Itazingatia uwezo wako za kipekee, rasilimali, vipaumbele, wasiwasi, ujuzi, mambo yanayokuvutia na uchaguzi ulioarifiwa.

### Jinsi na ni wakati gani Mpango wa Ajira Unaomlenga Mtu Binafsi huundwa?

Mara tu itakapobainika kuwa unastahiki kupokea huduma za Urekebishaji wa Kitaalamu, unaweza kuanza kuunda IPE yako. Lengo na huduma zinazohitajika katika mpango zinategemea pembejeo yako.  Hakikisha unajumuisha mambo yote yanayoathiri kazi yako.

Pia inategemea taarifa ambayo wewe au wengine watatoa kuhusu uwezo wako na mambo yanayokuvutia. Unakaribishwa kuhusisha familia, marafiki, wanachama wa mtandao wako wa msaada, watetezi, au wataalam kutoka nje ya DVR.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Baadhi ya mifano ya ujuzi na uwezo ni mawasiliano, kujipa motisha mwenyewe, kufanya maamuzi,<br><br>kufanya kazi vizuri chini ya shinikizo na kutumia wakati vizuri. |

### Je, ninawezaje kuunda Mpango wa Ajira Unaomlenga Mtu Binafsi ambao unanifaa mimi?

IPE huundwa kwa kukutana na VRC wako kujadili na kuchunguza uwezo wako, ujuzi, vipawa, mambo yanayokuvutia kikazi na uchaguzi ulioarifiwa.

Unaweza kurejelezwa kwa *Warsha ya Uchunguzi wa Kazi* kuchunguza mambo yanayokuvutia ya kitaalamu, taarifa za soko la ajira na mahitaji ya kazi.

Klabu ya Kazi ni fursa nyingine ya mwongozo kuhusu mada kama vile mahojiano, maombi ya kazi, wasifu na wakati wa kufichua taarifa kwa mwajiri.

Unaweza kuulizwa ukamilishe tathmini ya kitaalamu ili kuchunguza mambo yanayokuvutia kikazi. Mahojiano ya kutoa taarifa, uanagenzi wa kujifunza huku ukiwa kazini, ziara za kazi na uzoefu wa kazi ya kulipwa unaweza kuhimizwa kusaidia katika kuandaa IPE yako.

Rufaa zinaweza kupendekezwa kwa vipimo vya ziada vinanvyohusiana na ulemavu ili kutambua uwezo wa utendaji (kama vile vikwazo vya kuinua, nk) au kubaini ni marekebisho gani yanaweza kuhitajika katika eneo la kazi au mazingira ya elimu.

Ni muhimu kushiriki na mshauri wako wa VR misaada uliyonayo au unayoweza kuhitaji. Mfano wa mtandao wa msaada ni Clubhouse. DVR inafanya kazi kwa karibu na Clubhouses ambazo ziko katika Maine.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Warsha ya Uchunguzi wa Kazi (CEW) na Klabu ya Kazi ni shughuli mbili ambazo zinaweza kukuongoza katika njia yako ya kazi. |

### Kuamua kuhusu lengo la ajira

Kuna hatua mbili kuu za kuandaa IPE 1) kuamua kuhusu lengo la ajira na 2) kubaini jinsi utakavyofikia lengo hilo.

Kuna mambo mengi ambayo unapaswa kuzingatia wakati wa kuamua kuhusu lengo la ajira. Kwanza, ni ujuzi gani wa kazi ulio nao sasa? Ni aina gani ya kazi inayokufaa zaidi, kwa kuzingatia mambo kama ujuzi wako wa sasa, uwezo na mambo yanayokuvutia. Kisha angalia kazi yenyewe.

Baadhi ya maswali ya kuzingatia ni:

- Je, hii ni kazi yenye fursa nyingi za ajira?
- Waajiri watarajiwa wanapatikana wapi na je, usafiri utakuwa tatizo?
- Je, kutakuwa na fursa zipi za kujiendeleza kikazi?
- Je, kazi hii italipa kiasi gani, na je, hiyo kiasi hicho kinachokidhi mahitaji yako?
- Je, kuna unyumbufu katika mazingira ya kazi?
- Ni rasilimali gani utahitaji ili kufikia lengo lako?
- Ikiwa lengo litahitaji muda mwingi wa maandalizi, je, unaweza kumudu kutokuwa na ajira kwa muda mrefu wakati unapojitayarisha kwa lengo?

Wewe na mshauri wako wa VR mtachunguza njia za kazi. Njia ya kazi ni njia ya kupanga kazi. Kuunda njia ya kazi kunamaanisha kupanga mkakati wa kutambua mambo yanayokuvutia ya kazi, kubaini mahitaji ya elimu na mafunzo na kuanzisha mpango wa utekelezaji wa kufikia malengo ya kazi. Njia yako ya kazi itaelezwa kwa muhtasari kwenye IPE yako.

Mshauri wako wa VR anaweza kukusaidia kuchagua lengo la ajira linalokufaa. Mshauri wako wa VR ana taarifa kuhusu kazi mbalimbali, anaweza kujua watu wengine au shughuli ambazo zinaweza kukusaidia kupata taarifa zaidi na anaweza kusaidia kukuongoza katika mchakato wa kufanya uamuzi. Unaweza pia kuchagua kuhusisha watu kutoka nje ya DVR katika uendelezaji wa lengo lako la ajira.

Kwa maelezo zaidi kuhusu kuchagua lengo la kazi, angalia sehemu ya kijitabu hiki cha maelekezo inayoitwa, "Ninawezaje Kufanya Uchaguzi Mzuri wa Kazi?" katika sehemu ya Rasilimali kwenye ukurasa wa 22.

Kidokezo vya Kusaidia

Bonyeza viungo vifuatavyo kwa rasilimali muhimu za kukusaidia kuchunguza ajira:

Kituo cha Utafiti wa Kazi na Taarifa
Mtandao wa Marekebisho ya Ajira
Kituo cha Kazi cha Maine
O*Net
Huduma za Ajira na Usaidizi (Ofisi ya Huduma za Kuzeeka na Ulemavu)

### Kuandaa mpango wa kufikia lengo

IPE yako itaelezea huduma ambazo utahitaji ili kufikia lengo lako, muafaka wa muda, makaridio ya gharama ya lengo na huduma na majukumu ya kila mtu anayehusika katika mpango wako.

Huduma ambazo zimejumuishwa katika mpango huu zinapaswa kuwa zile tu ambazo ni muhimu kufikia lengo lako la ajira. Mambo unayopaswa kuzingatia ni pamoja na:

- Unahitaji nini ili kufikia lengo?
- Itachukua muda gani kufikia lengo hili?
- Ni njia ipi bora zaidi ya kufikia lengo, kwa kuzingatia muda na gharama?
- Ni kina nani watoaji wa huduma watarajiwa na ni yupi atakayekufaa zaidi?
- Je, utapata matatizo yoyote katika kufikia huduma unazohitaji (kwa sababu ya mambo kama vile usafiri, masuala yanayohusiana na ulemavu, nk)?

Mshauri wako wa VR ataweza kukusaidia kujua ni huduma gani unaweza kuhitaji kufikia lengo lako na anaweza kukuambia ni sheria gani za DVR zinatumika. Kwa huduma nyingi, Mshauri wako wa VR atakuwa na taarifa kuhusu ni nani anayeweza kutoa huduma unazohitaji. DVR inakuhimiza kuzungumza na watoa huduma na kupata taarifa zaidi

kutoka kwao kabla ya kuamua ni yupi wa kuchagua. Unaweza pia kuchagua kuhusisha watu wowote au vyanzo vyovyote kutoka nje ya DVR katika uundaji ya IPE yako.

IPE inaweza kuandikwa hadi mwaka mmoja. Kwa mfano, unaweza kutarajia kuwa na angalau IPE nne ikiwa unahudhuria programu ya shahada ya kwanza ya miaka minne. IPE pia inaweza kuandikwa kwa malengo ya muda mfupi, chini ya mwaka mmoja.

Mara tu wewe na Mshauri wako wa VR mtakapokubaliana kuhusu lengo lako la kazi na huduma unazohitaji kufikia lengo hilo, mpango wako unaweza kuandikwa, kutiwa sahihi na wewe na Mshauri wako wa VR na huduma zinaweza kuanza. Utapokea nakala ya IPE na marekebisho yoyote yaliyofanywa kwenye mpango. Marekebisho yanatokea ikiwa kuna mabadiliko yoyote yaliyofanywa kwenye mpango wako. IPE itasasishwa angalau mara moja kila mwaka.

| Vidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| *Ni muhimu kudumisha mawasiliano na VRC wako ili kuendeleza na kudumisha IPE yako. |
| *Njia mbadala ya kutia sahihi mpango wewe mwenyewe ni kupitia sahihi ya kielektroniki.<br>VRC wako atatoa maagizo kuhusu jinsi ya kufanya hivyo na nakala ya IPE yako. |
| *Hifadhi nakala ya IPE yako, IPE zote zinakaguliwa kila mwaka. |

### Mambo ambayo DVR inahitaji kuangalia kabla ya kukubaliana na IPE yako

DVR itaangalia mambo mengi na wewe ili kufikia makubaliano ya pamoja kuhusu IPE yako. Mambo makuu ambayo DVR itazingatia ni:

- Je, mpango huu unalingana na uwezo, rasilimali, vipaumbele, wasiwasi, uwezo, vipawa, mambo yanayokuvutia, na uchaguzi ulioarifiwa?
- Je, huduma zinazoombwa ni muhimu katika kufikia lengo lako?
- Je, taarifa za soko la ajira zinaunga mkono lengo lako katika eneo ulilochagua?
- Je, mpango huu utafuatiliwa vipi ili kuhakikisha matokeo yenye mafanikio?
- Je, muda wa utekelezaji ni muafaka kufikia lengo lako?
- Je, vyanzo vingine vya fedha vimechunguzwa, wakati inapofaa?
- Je, vyanzo vya malipo vimetambuliwa katika mpango?
- Je, huduma inatolewa kwa njia ya gharama nafuu zaidi?
- Je, matibabu au hatua za msaada ambazo unahitaji kufanikiwa zimeshughulikiwa katika mpango?
- Je, huduma zinalingana na kanuni na sera za DVR?

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Hakikisha unahudhuria miadi iliyopangwa. Kukosa miadi kunaweza kuchelewesha mpango wako.<br>Ikiwa ni lazima ughairi, piga simu mapema na upange upya miadi yako. |

### Je, nifanye nini ikiwa ninataka kubadilisha IPE yangu AU ikiwa ninahitaji huduma zaidi?

Ni muhimu kwamba uwasiliane na Mshauri wako wa VR mara moja ili kujadili mabadiliko yoyote katika IPE yako. Wakati mabadiliko yanakubaliwa, IPE itarekebishwa. Wewe na mshauri wako mtapitia na kusasisha mpango wako angalau mara moja kwa mwaka, hata kama hakuna mabadiliko makubwa.

Mshauri wako wa VR ni mtu muhimu unayeweza kwenda kwake ili kupata majibu. Utoaji wa huduma yoyote unategemea mahitaji ya mtu binafsi. Ikiwa mshauri wako hawezi kujibu maswali yako kwa njia inayokuridhisha, unapaswa kuomba kuzungumza na msimamizi wa DVR. Ikiwa bado haukubaliani na DVR, kuna taratibu zingine ambazo zinaweza kusaidia. Kwa taarifa zaidi kuhusu hili, rejelea "Ninafaa Kufanya Nini Ikiwa Sikubaliani na VR?" ukurasa wa 10 wa kijitabu hiki cha maelezo.

### Ni nani atakayelipia huduma ninazohitaji?

Kila mtu ana Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira tofauti. Unaelezea lengo la ajira, huduma zinazohitajika kufikia lengo hilo na makubaliano kati yako na DVR. Rasilimali nyingi zinaweza kutumika kufidia gharama za huduma chini ya Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira, ikiwa ni pamoja na rasilimali zako, rasilimali za familia yako, bima yako au manufaa mengine, mipango mingine ya umma na/au DVR. Kila Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira unapaswa kuelezea kwa uangalifu ni nani anayewajibika kulipa huduma gani.

Utaulizwa kuchangia rasilimali kwa hiari kusaidia kufidia gharama ya Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira. Mifano ya jinsi unavyoweza kuchangia rasilimali ni pamoja na: kulipa muuzaji sehemu ya gharama ya huduma unazohitaji, kutoa rasilimali zisizo za kifedha au kupata baadhi ya huduma peke yako. DVR inaamini sana kwamba mchango wa kibinafsi wa kila mtu ni kiungo muhimu katika kufanya Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira kuwa na maana na wenye mafanikio. Hata hivyo, si lazima utoe mchango, na mpango wako hauwezi kuzuiliwa ikiwa huna uwezo wa kuchangia.

Kabla ya fedha za DVR kutumika, tunahitaji kuangalia rasilimali zingine zinazopatikana. Je, kuna rasilimali zingine (kama vile mashirika mengine, bima yako ya afya, msaada wa kifedha kwa elimu ya juu, manufaa ya wafanyikazi) ambazo zitalipia huduma unazohitaji. Unaweza kuhitajika kutuma maombi kwa rasilimali hizi nyingine. DVR pia itatumia rasilimali nyingine zozote ambazo zinapatikana kwa urahisi kugharamia Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira.

DVR inaweza kulipia huduma au bidhaa ambazo hazipatikani kutoka vyanzo vingine na ambazo zimekubaliwa katika Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira. Bidhaa na huduma hizi lazima zinunuliwe kwa njia ambayo inakubaliana na sera za ununuzi za Jimbo na DVR. DVR inaweza kutumia tu watoa huduma ambao wanakubaliana na sera na masharti haya.

Unaweza kuchagua huduma ambazo DVR inaweza kupata kwa gharama nafuu zaidi mahali pengine, huenda ukalazimika kulipia tofauti hiyo.

Baadhi ya watu ambao hupokea Mapato ya Ziada ya Usalama (SSI) na/au Bima ya Ulemavu wa Usalama wa Jamii (SSDI) wanaweza kustahiki kwa mpango wa Tiketi ya Kazi (Ticket to Work). Utawala wa Usalama wa Jamii hutoa fidia ya malipo kwa DVR wakati wamiliki wa tiketi wanapata mapato kwa mshahara mkubwa.

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu ni nani anayelipa huduma katika Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira, tafadhali uliza Mshauri wako wa VR. Ni muhimu ujue ni nani anayelipa na ni gharama gani za huduma na bidhaa katika Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira. Maarifa haya yatakusaidia kufanya maamuzi bora kuhusu huduma unazopokea.

Kidokezo vya Kusaidia

Mifano ya manufaa linganishi ni; Msaada wa Kifedha, Bima ya Afya,

Usafiri wa Umma, Manufaa ya Wafanyakazi.

Bonyeza hapa kwa taarifa zaidi kuhusu Mpango wa Tiketi ya Kazi.

## Utakapofikia lengo lako la ajira

Mshauri wako wa VR atadumisha mawasiliano na wewe katika siku zako za kwanza tisini (90) kazini, au zaidi ikiwa ni inahitajika, ili kuhakikisha kazi yako inaridhisha. Kwa ruhusa yako, Mshauri wako wa VR anaweza kuwasiliana na msimamizi wako ili kujadili maendeleo yako kazini.

DVR inaweza kutoa msaada wa kiufundi kwako na mwajiri wako ili kutambua njia za kukidhi mahitaji yako yanayohusiana na ulemavu. Hii inaweza kujumuisha vifaa maalum au kupanga upya mazingira ya kazi.

Mara tu unapoajiriwa na kabla ya kufungwa kwenye mafanikio, huduma za baada ya ajira zinaweza kutolewa ikiwa huduma hizo zina upeo mdogo na muda mfupi. Huduma za baada ya ajira zimewekewa kikomo cha huduma moja au mbili katika kipindi cha chini ya miezi sita (6). Wewe na Mshauri wako wa VR mtarekebisha Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira ikiwa misaada wa baada ya ajira inahitajika. Ikiwa utapata changamoto katika kudumisha ajira yako, tafadhali wasiliana na Mshauri wako wa VR.

Ikiwa kesi yako ya VR imefungwa na unahitaji msaada wa ziada utahitaji kutuma maombi tena kwa huduma kwa kukamilisha fomu ya Maombi ya Urekebishaji wa Kitaalamu.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Baada ya kazi na kuimarika katika ajira yako DVR itasubiri angalau siku 90 kabla ya kufunga kesi yako. |

## Huduma ambazo DVR inaweza kutoa

Ifuatayo ni orodha ya aina za huduma ambazo DVR inaweza kutoa, ikiwa inahitajika kama sehemu ya IPE yako. Katika kijitabu hiki cha maelezo utapata taarifa zaidi kuhusu mada zilizo hapa chini. Unahimizwa kuuliza Mshauri wako wa VR au wafanyikazi wengine wa DVR ikiwa una maswali kuhusu upatikanaji au uhitaji la huduma yoyote. Mifano ya huduma za msingi imeorodheshwa hapa chini:

- Ushauri, mwongozo, na taarifa kuhusu maamuzi ya kazi na ajira
- Huduma za tathmini ili kubaini ustahiki na mahitaji ya urekebishaji wa kitaalamu. Kulingana na hali yako, hii inaweza kujumuisha vitu kama fursa za kuangalia maeneo halisi za kazi, kufanya kazi kwa kipindi cha majaribio, vipimo vya matibabu au kisaikolojia, au njia zingine za kujifunza zaidi kuhusu ulemavu wako na mahitaji ya urekebishaji wa kitaalamu.
- Rufaa kwenda kwa watoa huduma wengine kwa huduma ambazo hazipatikani kupitia mpango huu
- Huduma za uwekaji wa kazi
- Mafunzo ya ajira na huduma nyingine za mafunzo
- Huduma za urejeshaji wa kimwili na kiakili
- Huduma za kujiajiri, ikiwa ni pamoja na msaada wa kiufundi na ushauri wa kuanzisha shughuli ndogo ndogo za biashara
- Leseni za kazi, zana, vifaa, na bidhaa za kwanza na ugavi
- Teknolojia ya Urekebishaji / Teknolojia Saidizi
- Mafunzo ya kazi na huduma zingine za ajira zinazopatikana
- Huduma za mpito za kibinafsi kusaidia uhamaji kutoka shule hadi kazi
- Huduma za Mpito za Kabla ya Ajira kwa Wanafunzi wenye Ulemavu

### Huduma za Msaada

Huduma za msaada zinaweza pia kutolewa ili kusaidia huduma za msingi zilizotajwa hapo juu. Gharama zote za msaada zinahitaji kuwa za maana, muhimu na za gharama nafuu. Baadhi ya mifano ya huduma za msaada ni:

- Huduma kwa wanafamilia, ikiwa inahitajika kwa mtu mwenye ulemavu ili kufikia lengo la ajira
- Malipo ya gharama za ziada zilizopatikana wakati wa kushiriki katika tathmini ya DVR au Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira
- Huduma za usafiri
- Huduma za msaada wa kibinafsi. Hizi ni huduma zinazohitajika na mtu ili kusaidia katika kufanya shughuli za maisha ya kila siku kutokana na ulemavu ambazo ni muhimu kwa mtu kufikia lengo la ajira.
- Huduma za ukalimani au msomaji
- Huduma za baada ya ajira kusaidia watu kudumisha kazi zao, kupata kazi katika sekta hiyo au unayohusiana, au kuendeleza kazi zao

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Huduma zinazotolewa na VR lazima zifuate Kanuni ya Mpango. |
| Manufaa linganishi ni fedha zinazopatikana kupitia rasilimali zingine ambazo zinaweza kupatikana kusaidia kulipia baadhi ya huduma zilizoorodheshwa kwenye IPE yako. |

## Nini kitatokea kwa manufaa yangu ikiwa nitaenda kazini?

Ikiwa unapokea pesa taslimu au manufaa za matibabu kutokana na ulemavu (kama vile Bima ya Ulemavu wa Usalama wa Jamii, Mapato ya Ziada ya Usalama, Ruzuku ya Jimbo, Medicare na/au MaineCare, kuna vichocheo vya kukuhimiza kujaribu kufanya kazi wakati bado unapokea manufaa.  Ni muhimu kupata taarifa sahihi ili uweze kufanya maamuzi mazuri kuhusu malengo yako ya kitaalamu, mapato yako yanayowezekana na mahitaji yako ya bima ya afya KABLA ya kuanza mpango wa ajira.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Ikiwa wewe ni mpokeaji wa SSDI / SSI, hakikisha kuuliza kuhusu Gharama za Kazi Zinazohusiana na Ulemavu (IRWE - Impairment Related Work Expenses) |

### Ninawezaje kupata taarifa ambayo ninahitaji kuhusu manufaa ili niweze kufanya uchaguzi mzuri wa kitaalamu?

Manufaa ya kila mtu ni ya kipekee. Vichocheo vya kazi vinatumika kwa kila mtu kulingana na hali yake ya kibinafsi. Njia bora ya kupata taarifa sahihi kuhusu kazi na jinsi itakavyoathiri manufaa yako ni kuwasiliana na chanzo cha manufaa, kama vile Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu; Utawala wa Usalama wa Jamii; Nyumba za Jimbo la Maine; au wasiliana na Mtaalamu wa Manufaa ambaye ana mafunzo ya kina katika vichocheo vya kazi na programu zingine nyingi za manufaa.

Kituo cha Matibabu cha Maine kinatoa Huduma za Ushauri wa Manufaa kote jimboni. VRC wako atakusaidia kukamilisha fomu ya rufaa ili uweze kukutana na Mshauri wa Vichocheo wa Kazi ya Jamii (CWIC - Community Work Incentive Counselor). CWIC anaweza kujibu maswali yako kuhusu kazi na manufaa na atazungumza na wewe kuhusu vichocheo vya kazi vinavyopatikana kwako.

CWIC anaweza kufuta dhana potofu nyingi zinazohusiana na manufaa na kazi. Mara nyingi tunasikia kutoka kwa wapokeaji hofu waliyo nayo ya kupoteza SSI/SSDI na huduma ya afya, kama vile MaineCare au Medicaid. Kwa kukutana na CWIC, utapokea taarifa kuhusu jinsi hofu hizi mbili kuu ni dhana potofu. Kuna vichocheo vingi vilivyowekwa kuunga mkono uamuzi wako wa kufanya kazi. Pia utasikia kuhusu manufaa yaliyoongezwa ya kazi, kama vile, kuongeza mapato ya kila mwezi, kujenga mahusiano ya kijamii na kujitunza.

Mpango wa Tiketi ya Kazi hutolewa kupitia Utawala wa Usalama wa Jamii. Huu ni mpango wa hiari ulioundwa kusaidia watu ambao wanapokea manufaa ya ulemavu kutoka kwa Usalama wa Jamii katika kupata ajira yenye maana. Ikiwa unataka taarifa za ziada zungumza na Mshauri wako wa VR au Utawala wa Usalama wa Jamii.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Ikiwa wewe ni mpokeaji wa Manufaa ya Usalama wa Jamii utarejelezwa ili uonane na Mratibu wa Vichocheo vya Kazi ya Jamii (CWIC) kupitia Kituo cha Matibabu cha Maine ili kujadili manufaa na vichocheo vya kazi.<br>Taarifa zaidi zinapatikana kwa kutembelea Huduma za Ushauri wa Manufaa katika Kituo cha Matibabu cha Maine. |

## Nifanye nini ikiwa sikubaliani na DVR?

Ikiwa haukubaliani na uamuzi ambao DVR imefanya kukuhusu wewe, kuna chaguzi kadhaa za kutatua kutokubaliana huko. Hapa chini kuna maelezo ya baadhi ya chaguzi hizo ambazo zimeundwa kukusaidia wewe na DVR kusonga mbele katika kupanga urekebishaji wako wa kitaalamu.

Kujadili suala hilo kwa DVR. Ikiwa kuna kutokubaliana, DVR inakuhimiza kwanza kujadili wasiwasi wako na Mshauri wako wa VR. Hii inaweza kuwa njia ya haraka na rahisi zaidi ya kutatua tofauti yoyote. Ikiwa huwezi kutatua tofauti zako kwa kuzungumza na Mshauri wako wa VR, unaweza kutaka kujadili suala hilo na mwakilishi mwingine wa DVR, kama vile msimamizi, meneja wa eneo au meneja wa ofisi kuu ya DVR. Ofisi ya DVR ya eneo lako inaweza kukupa taarifa kuhusu jinsi ya kuwasiliana na mtu yeyote kati ya watu hawa.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Usisubiri, mjulishe VRC wako kujua ikiwa una maswali yoyote au haukubaliani na uamuzi. |

### Wasiliana na Mpango ya Msaada wa Wateja (CAP - Client Assistance Program )

Mpango wa Msaada wa Wateja (CAP) unaendeshwa na Haki za Ulemavu za Maine (DRM - Disability Rights Maine). CAP hutoa taarifa, ushauri, utetezi na, ikiwa itaonekana kuwa ni muhimu, uwakilishi wa kisheria kwa watu ambao wana wasiwasi kuhusu huduma za urekebishaji wanazopokea kutoka kwa DVR. CAP inahitajika kutumia njia zisizo rasmi, kama vile majadiliano, katika kutatua migogoro, kwa kiwango cha juu iwezekanavyo, kabla ya kutumia njia rasmi au za kisheria kama vile Upatinisho au Usikilizaji wa Utaratibu wa Haki. Kila kesi ni ya kipekee na, katika baadhi ya matukio, inaweza kuamuliwa kuwa njia pekee ya kutatua mzozo ni kwenda moja kwa moja kwa Upatinisho au Usikilizaji wa Utaratibu wa Haki.

Una haki ya kuomba njia yoyote ya kutatua kutokubaliana ndani ya siku thelathini (30) za mzozo, na au bila msaada kutoka kwa CAP. Ushauri wote na majadiliano na CAP ni ya siri na hayataathiri huduma zako vibaya.

Taarifa za mawasiliano za Haki za Ulemavu za Maine

Augusta
160 Capitol Street, Suite 4
Augusta, ME 04330
800-452-1948 (V / TTY)
207-626-2774 (V / TTY)
207-621-1419 (Faksi)
advocate@drm.org

Falmouth
1 Macworth Island, Building C
Falmouth, ME 04105
800-639-3884 (V / TTY)
207-797-7656 (V / TTY)
207-766-7111 (VP)
207-797-9791 (Faksi)
deafservices@drme.org

Ikiwa unataka kuomba msaada kupitia tovuti ya DRM, tembelea https://drme.org/online-intake-form.

## Taratibu za Utatuzi wa Migogoro:

Majadiliano kwa kawaida huhusisha kusaidia mawasiliano kati yako na Mshauri wako wa VR au kujadili njia tofauti za kutatua kutokubaliana. Majadiliano mara nyingi ni njia ya haraka zaidi ya kutatua tatizo.

Upatanisho ni mchakato wa hiari usio rasmi wa utatuzi wa mizozo ambapo mpatanishi, ambaye sio mfanyakazi wa DVR, anakusaidia wewe na DVR kufikia makubaliano. Mpatanishi hana mamlaka ya kufanya uamuzi kwa niaba yako au ya DVR. Ikiwa unafikia makubaliano na DVR, makubaliano hayo yatawekwa katika maandishi na kutiwa sahihi na wewe na DVR. Utapokea nakala ya makubaliano huu. Aina hii ya utatuzi wa mizozo inaweza kutolewa tu ikiwa wewe na DVR mnakubali kushiriki Upatanisho.

Katika Usikilizaji wa Utaratibu wa Haki, utawasilisha taarifa kuhusu mgogoro wako kwa afisa wa kusikiliza kesi, ambaye sio mfanyakazi wa DVR. Mchakato huu ni rasmi zaidi na taarifa iliyowasilishwa na wewe na DVR kwa kawaida ni ya kina zaidi kuliko katika Upatanisho. Katika Usikilizaji wa Utaratibu wa Haki, wewe na DVR kawaida huwakilishwa na mawakili au wanasheria na mnaweza kuwaita mashahidi. Mchakato wa kupanga, kufanya kikao na kufanywa kwa uamuzi na afisa wa kusikiliza kesi kwa kawaida huchukua muda mrefu zaidi kuliko kwa Mapitio yasiyo Rasmi. Ikiwa haukubaliani na uamuzi wa afisa wa kusikiliza kesi, unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi kupitia mfumo wa mahakama.

Maombi ya Upatanisho na Usikilizaji wa Utaratibu wa Haki lazima yawe kwa maandishi na kutumwa kwa Mkurugenzi wa DVR. Anwani ya Ofisi ya Utawala ya DVR inaweza kupatikana mwishoni mwa kijitabu hiki. Ikiwa unaamua kuwa unataka kupitia mojawapo ya taratibu hizi, DVR lazima ipokee ombi lako ndani ya siku thelathini (30) baada ya DVR kukujulisha kuhusu uamuzi ambao haukubaliani nao.

Katika yoyote kati ya taratibu hizi, una haki ya kuleta mwakilishi (kwa mfano, wakili wa CAP, wanasheria, mwanafamilia, nk). Hata hivyo, DVR haitawajibika kwa gharama za kuleta mwakilishi wako (kama vile ada inayotozwa na wakili wa kibinafsi).

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Maombi ya Upatanisho na Usikilizaji wa Utaratibu wa Haki lazima yawe kwa maandishi na kutumwa kwenye Ofisi ya Utawala kwa uangalizi wa Mkurugenzi wa DVR |

# Huduma za DVR

## Uzoefu wa Kazi ya Kulipwa

Uzoefu wa kazi ya kulipwa ni fursa kwako kujaribu kazi moja au zaidi katika jamii. Uzoefu wa kazi ya kulipwa unaweza kukusaidia kujifunza zaidi kuhusu kazi zinazolingana na mambo yanayokuvutia na ujuzi wako au inaweza kukusaidia kujenga historia yako ya kazi. Uchaguzi wa kazi utategemea mambo yanayokuvutia, ujuzi, na mahitaji yako. Uzoefu wa kazi unaweza kutofautiana kwa muda kulingana na hali yako, utalipwa kwa kazi unayofanya wakati wa uzoefu huo, kwa kawaida kwa kiwango cha mshahara wa kawaida cha nafasi hiyo. Mishahara hulipwa kupitia shirika la muda ambalo lina mkataba na VR.

Wakati inapokubaliwa kuwa utafaidika na uzoefu wa kazi ya kulipwa, Mshauri wako wa VR atatambua ni misaada gani inahitajika ili kupata nafasi ya ajira. Hii inaweza kujumuisha kufanya kazi na wafanyikazi wengine wa DVR au rufaa kuenda kwa Mtoa Huduma wa Urekebishaji wa Jamii. Kabla ya uzoefu wa kazi kuanza, unahitaji kushiriki katika uamuzi kuhusu aina ya kazi utakayokuwa unafanya. Ni muhimu kuwamjulisha mshauri wako wa VR na mtaalamu wa tathmini kuhusu chochote kinachoweza kuwasaidia kupata mahali panapofaa pa uzoefu wa kazi.

Kabla na wakati wa uzoefu wa kazi, ni muhimu kwako kuelewa kile kinachotarajiwa kutoka kwako. Kuhudhuria kuzuri katika mikutano ya kupanga na kazini, kufika kwa wakati, mavazi yanayofaa na kuwa na mahusiano mazuri na mwajiri pamoja na wafanyakazi wenzako, itakuwa muhimu kila wakati. Aidha, kazi unayofanyiwa tathmini inaweza kuwa na mahitaji mengine ambayo unapaswa kujua.

Mara tu uzoefu wa kazi unapokamilika wewe na VRC wako mtajadili matokeo ya kubaini hatua zifuatazo. Maoni yako kuhusu uzoefu wa kazi ni muhimu kuendeleza hatua zifuatazo. Pamoja, wewe na Mshauri wako wa VR mtaangalia mambo mengi ya utendaji wako wa kazi kama vile: ujuzi wako wa kazi, tabia, uhusiano na mwajiri na wafanyikazi wenzako, mahudhurio, na uvumilivu wa kazi. Kupitia kushiriki katika uzoefu wa kazi ya kulipwa, utakuwa na nafasi ya kuona jinsi unavyopenda kazi na jinsi unavyoimudu. Uzoefu wa kazi unaweza kupangwa na mwajiri ambaye ana nafasi ya kazi, na ikiwa wameridhika na kazi yako, unaweza kupewa kazi. Baada ya uzoefu wa kazi kukamilika, wewe na mshauri wako mtapata ripoti kutoka kwa mtaalamu wa tathmini akielezea jinsi ulivyofanya, ikiwa kazi inaonekana kuwa inakufaa na ikiwa utahitaji huduma zingine ili kufanikisha ajira yako.

Hatimaye, ni muhimu kwako kuuliza maswali yoyote ambayo unaweza kuwa nayo na kutoa maoni wakati wa mchakato.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Maeneo ya uzoefu wa kazi yataamuliwa na mambo yanayokuvutia, uwezo wako, mahitaji ya mwajiri na chaguzi za usafirishaji. |
| Wakati mwingine uzoefu wa kazi ya kulipwa unaweza kupelekea ajira ikiwa kazi hiyo inakufaa |

Wakati wewe na Mshauri wako wa VR mnaamua kwamba uko tayari kutafuta kazi, Mshauri wako wa VR atafanya kazi na wewe kutafuta ajira au kupanga huduma zingine, ikiwa ni inahitajika, kukusaidia kupata kazi.
Kutafuta kazi kunahitaji juhudi kubwa. Ili kufanikiwa kupata kazi unayotaka, itakuwa muhimu kwako kufanya sehemu yako. Kadiri unavyozidi kutafuta kazi zaidi, ndivyo nafasi zako za kupata ajira zinavyoongezeka. Baadhi ya mambo unayoweza kufanya ni kujiandikisha katika Maine Job Link, huduma ya Idara ya Kazi CareerCenter, na upitie tovuti za utafutaji wa kazi. Kuna huduma kadhaa ambazo DVR inaweza kukupa ili kukusaidia katika kupata ajira, kulingana na mahitaji yako, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- Ujuzi wa Kutafuta Kazi (JSS-Job Seeking Skills) - JSS hutoa msaada na ujuzi wa mahojiano: uandishi wa wasifu na mbinu za kutuma maombi kukusaidia kujiandaa kwa utafutaji wako wa kazi. JSS inaweza kuwa msaada wa kibinafsi au kutolewa kama sehemu ya darasa

- Msaada wa Kupata Kazi wa Kibinafsi - Mshauri wako wa VR anaweza kukusaidia kutambua waajiri wa eneo lako ambao wanaweza kuwa na fursa za kazi katika eneo lako la mambo yanayokuvutia au kukushauri kuhusu mahojiano na uandishi wa wasifu. Ikiwa inahitajika, mipango inaweza kufanywa ili mtu aandamane kwenda katika mahojiano
- Marejeleo kwa warsha kama vile kuandika wasifu na ujuzi wa mahojiano
- Nafasi za kazi za eneo lako, ufuatiliaji na waajiri, na msaada unaoendelea
- Uzoefu wa kazi ya kulipwa- Uzoefu wa kazi ya kulipwa ni fursa kwako kujaribu kazi ili kubaini ikiwa aina hiyo ya kazi inakufaa
- Kocha wa kazi anaweza kuandamana nawe kukusaidia katika kujifunza kazi na kufuatilia utendaji wako. Mwajiri anaweza kukupa kazi ikiwa utaonyesha utendaji mzuri wakati wa tathmini
- Programu ya Uanagenzi ya Maine, kwa kushirikiana na DVR, husaidia katika kuandaa programu za mafunzo zilizopangiliwa lakini zinazonyumbufu ambazo zimeundwa kujumuisha mafunzo ya kazini mafundisho ya darasani yanayohusiana
- Warsha ya Uchunguzi wa Kazi (CEW) ni darasa ambapo utachunguza maeneo ya ajira unayovutiwa nayo, na pia kugundua ujuzi na talanta ambazo ni za kipekee kwako. Warsha hii mara nyingi hufanyika katika CareerCenter cha eneo laki, shule, au shirika mshirika. Inaweza kuwezeshwa na wafanyikazi wa DVR au kwa kushirikiana na wengine
- Klabu ya Kazi ni mkutano wa kikundi kidogo wa mtandaoni unaosaidia utafutaji wako wa kazi. Maeneo kadhaa ya mada yanashughulikiwa, na washauri wanapatikana kujibu maswali yanayohusiana na maeneo haya ya mada
- Mafunzo ya Kazini (OJT-On- the- Job Training) ni mpangilio kati ya mwajiri na DVR ambapo mwajiri anakubali kuajiri mtu na kumpa mafunzo huku DVR ikisaidia na gharama za kwanza za mafunzo na msaada. Baada ya mwajiri kupatikana mkataba wa maandishi utaandaliwa kati yako, mwajiri na DVR. Mkataba huu utajumuisha mshahara wa saa utakaolipwa kutoka kwa mwajiri, masaa ya mafunzo utakayopokea, na muda utakaochukua kupata ujuzi wa kiwango cha kuingia kazini.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Kujenga mahusiano na familia na marafiki mara nyingi kunaweza kusaidia kupata fursa za kazi. |
| Bonyeza hapa kwa maelezo zaidi kuhusu Programu ya Uanagenzi ya Maine |
| Warsha ya Uchunguzi wa Kazi na Klabu ya Kazi ni shughuli mbili za vikundi vidogo ambazo zinaweza kukusaidia katika kutambua njia yako ya kazi. |

Mshauri wa VR atafanya kazi na wewe ili kubinafsisha huduma ili kukidhi mahitaji yako, kama ilivyokuwa katika kesi ya Ryan:

*"Ryan", kijana mwenye historia ya kushindwa kupata ajira, alifanya kazi na VRC na Mtoa Huduma wa Urekebishaji wa Jamii kupata ajira inayomfaa kulingana na mahitaji yake. Aliimarika katika uwezo wake wa kupokea maoni yanayosaidia na sasa ana uhusiano mzuri na mwajiri wake na wafanyikazi wenzake. Hivi karibuni alimwambia VRC wake "Sihisi huzuni tena.".*

## Mafunzo ya Kazi na Ajira Zingine Zinazopatikana

### Mafunzo ya kazi ni nini?

Kocha wa Kazi ni mtu ambaye hutoa msaada wa ajira ulioibinafsishwa. Unaweza kuhitaji Kocha wa Kazi kwa muda mrefu au muda mfupi. Kocha wa Kazi kwa kawaida kukutana na wewe kazini lakini anaweza kukutana na wewe katika jamii kama hiyo ni sahihi na inakustarehesha wewe.

Baadhi ya mifano ya jinsi Kocha wa Kazi anaweza kukusaidia ni:

- Kukusaidia kujifunza ujuzi unaohitajika kwa kazi hiyo
- Kukusaidia kufanya kazi na wasimamizi na wafanyikazi wenzako
- Kukusaidia kujifunza jinsi ya kutumia usafiri kwa ajili ya kwenda kazini
- Kukusaidia kujua nini kinatarajiwa kutoka kwako kazini
- Kutoa msaada ikiwa kazi itakuwa ngumu sana kwako au ikiwa matatizo mengine yanatokea ambayo yanaathiri kazi yako

Kocha wa Kazi atafanya kazi na mwajiri ili kuhimiza usaidizi wa asili kazini. Usaidizi wa asili kwa kawaida hutolewa na mfanyakazi mwenzako au msimamizi ambaye anakuza uhusiano wa ushauri. Usaidizi wa asili huruhusu kupunguza msaada wa kocha wa kazi polepole na hivyo huongeza mtiririko wa asili kwenye eneo la kazi na kuongeza uhuru kwa mfanyakazi.

| |
|---|
| Kidokezo vya Kusaidia |
| Lengo la kila Kocha wa Kazi ni kukusaidia kujitegemea kazini. |
| Kocha wa Kazi atafanya kazi na wewe na mwajiri kupunguza/kutoa msaada wa mafunzo ya kazi wakati inafaa. |

### Ajira Inayosaidiwa

Ajira Inayosaidiwa ni kazi katika jamii yenye msaada unaoendelea (kwa kawaida mafunzo kazini) ili kukusaidia kudumisha kazi. Imeundwa kuwalenga watu ambao, kwa sababu ya ulemavu mkubwa, wanatarajiwa kuhitaji misaada kwa muda mrefu wanapoendelea kufanya kazi. Kiasi cha msaada ambacho utapokea kila siku au kila wiki kitategemea mahitaji yako. DVR inaweza kutoa huduma hizi kwa muda maalum pekee. Kwa sababu watu walio katika ajira inayosaidiwa watahitaji misaada wa muda mrefu, mipango lazima ifanywe kuhusu ni nani atakayetoa mafunzo ya kazi au misaada mingine baada ya huduma za DVR kukamilika. Kwa hakika, sheria inahitaji kwamba mipango hii ifanywe kabla ya mtu kuanza kufanya kazi katika ajira inayosaidiwa.

Kwa hivyo, ni muhimu sana kwamba ufanye kazi na mshauri wako kutuma maombi kwa huduma zingine ambazo zinaweza kupatikana ili kutoa msaada unaoendelea baada ya huduma za DVR kukamilika. Mifano ya rasilimali ambazo zinaweza kupatikana kutoa misaada hii inayoendelea ni: msaada wa asili kutoka kwa mwajiri; msaada wa kifamilia; Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu; Gharama za Kazi Zinazohusiana na Ulemavu za Usalama wa Jamii; na Fedha za Msaada Wa Muda Mrefu wa Msingi na Majeraha ya Ubongo wa DVR.

## Wakati lengo lako la ajira linahitaji Mafunzo

### Mafunzo ya Ajira ni nini?

Ni njia ambayo mtu hujifunza ujuzi unaohitajika kufanya kazi fulani au aina ya kazi. Mifano ni pamoja na:

- Mafunzo ya uanagenzi
- Uzoefu wa kazi unaolipwa
- Mafunzo ya ukiwa kazini
- Mafunzo maalum ya ujuzi maalum
- Mafunzo ya Ukufunzi
- Shule ya Kitaalamu/Kiufundi
- Mafunzo ya chuo

### Je, DVR inaweza kusaidia na mafunzo ya ajira?

Ikiwa mafunzo yanahitajika ili kufikia lengo lako la kazi, na ikiwa DVR imekubali kukusaidia na hii kama sehemu ya makubaliano ya pande zote kuhusu Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira, DVR inaweza kusaidia na mafunzo ya ajira. Aina ya mafunzo ambayo DVR itasaidia itategemea uwezo wako na mambo yanayokuvutia, taarifa kuhusu soko la ajira na utafiti kuhusu jinsi watu wengi wanavyoingia katika aina ya kazi unayotaka kufanya.

Njia za Kazi ni "ramani" ambazo zinaelezea kwa mukhtasari elimu na mafunzo ambayo lazima yakamilishwe na vyeti unavyopaswa kupata ili kufikia lengo lako la kazi. VRC wako atakusaidia katika kuunda mpango wa kazi wa kibinafsi au "ramani" ambayo inaonyesha hatua za kufikia malengo yako. Hatua hizi zitaelezewa kwa mukhtasari kwenye IPE yako.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| VR inaweza kusaidia tu mafunzo/elimu kutoka taasisi iliyoidhinishwa. |

## Ni nini kinachotarajiwa kutoka kwangu ikiwa DVR itanisaidia katika elimu ya juu?

- Wewe na Mshauri wako wa VR lazima mkubaliane kuhusu lengo lako la ajira na ikiwa mafunzo yanahitajika ili kufikia lengo hilo
- Unapaswa kutuma maombi na kukubaliwa kuingia katika programu ya mafunzo au shule unayotaka kuhudhuria
- Ikiwa unatuma maombi kwa chuo au taasisi nyingine ya elimu ya juu, lazima utume maombi ya msaada wa kifedha na ufuate taratibu na ratiba za shule. Unahitaji kuarifu DVR kuhusu mahitaji yoyote yanayohusiana na ulemavu ambayo utakuwa nayo wakati unahudhuria programu
- Lazima udumishe mahitaji ya utendaji wa shule au programu ili kubaki katika msimamo mzuri
- Unahitaji kujadili mabadiliko yoyote makubwa na Mshauri wako wa VR mapema kwa sababu Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira unaweza kuhitaji kurekebishwa
- Lazima utoe nakala za alama zako au ripoti za maendeleo kwa VR na kudumisha mawasiliano ya mara kwa mara na Mshauri wako wa VR

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Unaweza kutuma maombi ya Maombi ya Bila Gharama kwa Msaada wa Kifedha Wanafunzi wa Serikali Kuu (FAFSA-Free Application for Federal Student Aid) mapema kama mwezi Oktoba. |
| Ikiwa unatafuta malazi wasiliana na ofisi ya ulemavu ya shule yako kabla ya kila muhula kuanza. |

Tafadhali rejelea “Urekebishaji wa Kitaalamu, Elimu ya Juu, Mafunzo na Wewe: Mwongozo wa Mtumiaji” kwenye ukurasa wa 24.

*Bidii ya "John" na misaada ya VR vimemuweka kwenye njia nzuri ya kazi:*

*VRC alifurahi kushiriki kwamba kijana mwenye Ulemavu wa Kujifunza, ambaye amekuwa akifanya kazi naye, hivi karibuni alihitimu kutoka chuo na shahada ya Sayansi ya Mazingira. Kwa sababu hakuwa na msaada wa kifamilia, huduma za VR zilikuwa muhimu sana katika kumsaidia kukamilisha elimu yake. Habari njema zaidi, tayari ameajiriwa kwa kazi ya majira ya joto huko California kama Mtaalamu wa Mazingira wa Kibiolojia!*

## Huduma za Kujiajiri

Kujiajiri ni aina ya kazi ambapo unamiliki na kuendesha biashara yako mwenyewe. Inaweza kuwa biashara unayoendesha kutoka nyumbani kwako. Inaweza pia kuitwa biashara ndogo au biashara ndogo ndogo.

Ikiwa lengo lako la ajira linaweza kufikiwa vyema kupitia kujiajiri, DVR inaweza kukusaidia kuanzisha au kudumisha biashara.

Huduma za kujiajiri zinazotolewa na DVR ni kwa ajili ya huduma za kuanza na bidhaa pekee. Mifano inaweza kujumuisha washauri wa biashara, uhasibu, utangazaji, bidhaa za kuanza, bima, vibali, ada, vifaa vya kazi, kodi, malipo ya huduma za umma, usafirishaji, simu na gharama za posta.

Kwa ujumla, kuanzisha biashara yako mwenyewe kutahitaji kujitolea kwa muda wako na rasilimali zako ili kufanikiwa. Idara inaweza kukusaidia katika ukuzaji wa kujiajiri au biashara ndogo chini ya masharti yafuatayo.

Mahitaji ya DVR kwa mipango ya biashara ndogo:

- Utahitajika kukamilisha dodoso la kujiajiri.
- Lazima utengeneze Mpango wa Biashara na lazima uidhinishwe na Mshauri wa Biashara Aliyeidhinishwa, kama vile Kituo cha Maendeleo ya Biashara Ndogo cha Maine (SBDC-Maine Small Business Development Center), kama pendekezo linalofaa kiuchumi. Rasilimali mbadala ya biashara ndogo inayokubalika kwako na Mshauri wako wa VR inaweza kutumika badala ya SBDC. Ikiwa unahitaji msaada wa ziada, kuna Vituo vingi vya Ushauri wa Maendeleo ya Biashara Ndogo vinavyotoa ushauri na warsha zinazoendelea. Mshauri wako wa VR atakusaidia kupata mahusiano haya.
- Kabla ya kutoa huduma chini ya Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira kupitia lengo la kujiajiri, Idara lazima ikubali lengo na mpango wa biashara. Kwa kawaida DVR huweka kikomo kwenye mchango wake kuelekea kuanzisha biashara ndogo (ukiondoa mafunzo na gharama zinazohusiana na ulemavu) hadi $ 7,500 kwa biashara ambayo itakuruhusu kujitegemea kabisa au hadi $ 2,500 ambayo itakuruhusu kufanya kazi kwa muda maalumu na kuendelea kupokea manufaa kama SSI au SSDI
- Utatarajiwa kutafuta ufadhili wa nje kwa gharama za kuanza biashara yako, na lazima uchangie biashara yako kwa pesa taslimu, kazi ya mikono, na/au vifaa.
- Unatarajiwa kumiliki na kuendesha angalau 51% ya biashara hiyo
- Ujumbe muhimu: Mipango ya kujiajiri ambayo inatarajiwa kupelekea wewe kujitosheleza (kuweza kuwacha kutegemea manufaa yote ya umma) inahitaji uwe na *rekodi nzuri ya mkopo*, au historia wa kusimamia deni lako vizuri

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Kumbuka kwamba kuanza mpango wa kujiajiri kutachukua muda kuendelezwa. |
| Bonyeza hapa kwa Kituo cha Maendeleo ya Biashara Ndogo cha Maine. Vinjari kwa warsha na rasilimali. |

### Mara tu biashara ndogo inapoanza kufanya kazi:

Mshauri wako wa VR atatembelea eneo la biashara na/au atawasiliana nawe ili kuona jinsi biashara inavyoendelea. Kabla ya DVR kufunga kesi yako na shirika, wewe na Mshauri wako wa VR mtahitaji kuamua ikiwa bado unakubali kuwa biashara hiyo ni au itakuwa yenye mafanikio. Ili kukusaidia kufanikiwa, kipindi kilichopendekezwa cha ufuatiliaji wa watu walio kwenye mipango ya kujiajiri ni miaka miwili (2).

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Kesi yako ya VR kwa kawaida itakuwa wazi kwa muda mrefu chini ya mpango wa kujiajiri. |

## Huduma za Vijana za DVR

### Mipango ya mpito kutoka shule kwenda kazini

Idara ya Urekebishaji wa Kitaalamu (DVR) inajua umuhimu wa kuanza mapema na uchunguzi na maandalizi ya kazi. Tunawapa wanafunzi, vijana na watu wazima wachanga fursa za kujifunza kuhusu wao wenyewe na nguvu zao wakati wa kujenga ujuzi ambao utawasaidia kuingia katika ulimwengu wa kazi. VR inaamini kuwa mojawapo ya njia bora kwa vijana kujifunza kuhusu jinsi ujuzi wao na mambo yanayowavutia yanalingana na fursa za kazi ni kupitia uzoefu wa kazi unaolipwa katika jamii zao.

| Kidokezo vya Kusaidia |
|---|
| Hadi umri wa miaka 18 mlezi/mzazi wako atahitaji kutia sahihi makaratasi yote. |

### Huduma za Mpito za Kabla ya Ajira

VR inatoa Huduma za Mpito za Kabla ya Ajira (Pre-ETS) kwa wanafunzi wenye ulemavu, wenye umri wa miaka 14-21 (kuanzia darasa la 9^na kuendelea) ambao wametuma maombi na kupatikana wanastahiki huduma za VR au ambao wamekamilisha Fomu ya Usajili wa Pre-ETS. Pre-ETS hutolewa hasa kwa vikundi vya vijana kwa kushirikiana na shule na mashirika mengine na imeundwa kusaidia wanafunzi wenye ulemavu kujiandaa kwa ajili ya elimu ya juu na ajira.

Pre-ETS inajumuisha:

- Ushauri wa uchunguzi wa kazi
- Uzoefu wa kujifunza unaofanyika kazini, ambao unaweza kujumuisha fursa za shuleni au baada ya shule, uzoefu nje ya mazingira ya kawaida ya shule, na/au ukufunzi
- Ushauri kuhusu fursa za kujiandikisha katika mipango ya kina ya mpito au ya elimu ya juu
- Mafunzo ya utayari wa mahali pa kazi ili kuendeleza ujuzi wa kijamii na maisha ya kujitegemea
- Maelekezo ya kujitetea binafsi

Ikiwa mwanafunzi au kijana mwenye ulemavu anahitaji huduma zaidi za mpito zilizobinafsishwa kuliko Huduma za Mpito za Ajira za Kabla, basi DVR inapendekeza kwamba wakamilishe maombi ya huduma za VR wakiwa na umri wa miaka 16 au miaka miwili kabla ya kuhitimu shule ya sekondari au kutoka shuleni.

| Kidokezo vya Kusaidia |
|---|
| VR inaweza kukusaidia kuanza kufikiria kuhusu kazi kupitia Warsha ya Mpito ya Uchunguzi wa Kazi (TCEW), Njia ya Uchunguzi na rasilimali zingine nyingi. |

### Huduma Zipi Zinazotolewa na VR?

Baada ya kupatikana kuwa wanastahiki huduma za VR, vijana na watu wazima wachanga wanaweza pia kufanya kazi na Mshauri wao wa VR ili kuunda Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira (IPE). Mshauri wako wa VR anaweza:

- Kushiriki katika mikutano ya timu ya Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Elimu (IEP), hasa wakati lengo la mkutano ni kuhusu huduma za mpito. Mipango ya mpito inafanya kazi vizuri zaidi wakati malengo na madhumuni kutoka kwa Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira wa VR (IPE) unasaidia malengo ya baada ya shule ya sekondari kwenye IEP yako
- Pata kukujua wewe na familia yako ili uwe na ufahamu wa jinsi unavyoweza kufanya kazi na VR kabla na baada ya kuhitimu
- Kushauriana na wewe, familia yako na wafanyakazi wa shule kukusaidia kuchagua kozi shuleni ambazo zitakusaidia kufikia malengo yako ya baada ya shule na pia kukuza fursa za uzoefu wa ajira ukiwa bado shuleni

- Kukusaidia wewe na familia yako katika kufahamu, kupanga na kufikia mipango ya huduma ya watu wazima inayohusiana na ajira inayohitajika
- Kukualika kushiriki katika mtaala wa Warsha ya Uchunguzi wa Kazi ya Mpito ili kukusaidia kujifunza zaidi kuhusu nguvu na ujuzi wako
- Kukupa Huduma za Ushauri wa Rika kukusaidia kujiandaa kwa kazi yako ya kwanza au elimu ya juu
- Kuchunguza elimu ya kifedha, ushauri wa manufaa, teknolojia ya urekebishaji na mahitaji mengine
- Kupanga mahojiano ya taarifa, uanagenzi wa kujifunza huku ukiwa kazini, na uzoefu wa kazi unaolipwa katika jamii

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Kufanya kazi kwa karibu na VRC wako kutakusaidia kuchunguza fursa za chaguzi za ajira sasa na baadaye. |
| Bonyeza hapa kwa Mwongozo wa Huduma za Mpito wa Maine na Pata Njia Yako ya Ajira |
| Bonyeza hapa kwa Mwongozo wa Elimu ya Kifedha |

*“Sandy” alipata matokeo yasiyotarajiwa ya kushiriki katika ziara ya kazi:*

*Sandy” alijiunga na ziara ya kikundi katika kituo cha makazi ya wazee huko Lewiston. Ziara hii ilipelekea fursa ya mahojiano ambayo hatimaye yalimletea ofa ya kazi! Amefurahi sana kuanza kazi yake mpya kama msaidizi wa lishe.*

## Ajira Inayoendelea

Baada ya kupatikana kuwa wanastahiki huduma za Urekebishaji wa Kitaalamu, vijana na familia zao hujadiliana na mshauri wao wa VR waliyepewa kujua ikiwa Ajira Inayoendelea ndio njia sahihi. Vijana ambao wanarejelewa kwa Ajira Inayoendelea hufikia timu ya wataalamu wa ajira kwa vijana ambao wanashiriki maarifa yao na kuunda mawazo katika mikutano ya mara kwa mara ya wafanyakazi- hii hupelekea fursa zaidi!

Fursa za shughuli za mikono katika jamii hujumuisha:

- Ziara ya Kazi
- Mahojiano
- Uanagenzi wa kujifunza huku ukiwa kazini
- Uzoefu wa Kazi/Uzoefu wa Kazi wa Majira ya Joto
- Mafunzo ya ukiwa kazini

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Ajira Inayoendelea inakuruhusu kushiriki katika fursa za kitaalamu wakati uko tayari! |

Bonyeza hapa kutazama Safari za Mitchell na Gabby za Ajira Inayoendelea.

*Ajira Inayoendelea ilimsaidia "John" kushiriki hatua kwa hatua katika shughuli za ajira kwa kasi yake mwenyewe:*

*"John", kijana mwenye Tawahudi alihitimu kutoka shule ya upili mwaka uliopita akiwa na nia ya kufanya kazi katika huduma za chakula. Familia ya John ilikuwa na wasiwasi mkubwa kuhusu kumruhusu aende mahali popote peke yake na watoa huduma waliokuwa wanafanya kazi naye walishangaa jinsi hali hiyo ingeathiri ufikiaji wake wa ajira.  John alielekezwa kwenye Mtindo wa Ajira Inayoendelea wa DVR na akaanza kufanya kazi na Mshauri wa Kazi. Mshauri wa Kazi alimchukua kwa mwendo wa taratibu na baada ya muda akapata imani ya mteja na familia yake. Baada ya shughuli kadhaa, John aliajiriwa katika mgahawa wa eneo lake akifanya maandalizi ya chakula na sasa anajifunza kutumia mashine ya malipo pia. Yeye ni mfanyakazi anayependwa sana na anayethamaniwa. Cha kusisimua pia, sasa anapanda basi mwenyewe kwenda kazini!*

## Teknolojia ya Urekebishaji/ Teknolojia Saidizi

Teknolojia ya Ukarabati, wakati mwingine pia inajulikana kama Teknolojia ya Kusaidia, ni tathmini na matumizi ya vifaa vinavyosaidia watu wenye ulemavu kudumisha au kuboresha uwezo wao wa kufanya kazi kwa kujitegemea. Teknolojia ya Urekebishaji pia inajumuisha huduma zozote zinazohitajika kupima, kujaribu, au kujifunza matumizi ya vifaa. Katika urekebishaji wa kitaalmu, Teknolojia ya Urekebishaji hutumiwa kwa madhumuni ya kusaidia watu kufanya kazi kwa kujitegemea zaidi au kushiriki kwa kujitegemea zaidi katika Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira na kupelekea ajira nzuri.

Kuna aina nyingi za vifaa vya teknolojia. Baadhi ya vifaa hivi ni rahisi na vyepesi kama vile funguo, mwongozo wa kuandika kwa karatasi, kiookuzi, au kibodi iliyobadilishwa. Vingine ni changamani zaidi na vinaweza kuhitaji mafunzo ili kuvitumia. Mifano inajumuisha kompyuta iliyo na programu ya kutambua sauti, kiti cha magurudumu chenye nguvu za kujiendesha au skuta, viungo bandi na vifaa vya usaidizi wa mwil (viungo vya bandia, gango), vifaa vya kusikia na vifaa vingine vya mawasiliano, na marekebisho ya gari.

Mshauri wako wa VR atafanya kazi na wewe kubaini ikiwa unahitaji vifaa au huduma zozote za Teknolojia ya Urekebishaji. Tathmini ya mtaalamu wa teknolojia (mtaalamu kutoka nje ya DVR) inaweza kutolewa ili kukusaidia katika kujifunza teknolojia gani inapatikana na jinsi inaweza kuboresha utendaji wako unapofikiria kuhusu mipango na malengo yako ya kazi au jinsi kazi maalum inaweza kubadilishwa kwa mahitaji yako.

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Ikiwa tayari unafanya kazi na mtaalamu aliyehitimu kuleta hati kwa VRC wako. |
| Teknolojia saidizi imebinafsishwa na itatofautiana kulingana na IPE yako. |

### Je, ni mchakato gani wa kupata huduma za teknolojia ya urekebishaji?

1. Wewe na Mshauri wako wa VR mnaweza kukubaliana kuhusu vifaa rahisi ambavyo vinaweza, kwa kawaida, kununuliwa haraka na kwa urahisi.
2. Wakati wewe na Mshauri wako wa VR mnaamua kwamba unahitaji Ushauri wa Teknolojia ya Urekebishaji, Mshauri wako wa VR atakuelekeza kwa mtaalamu wa teknolojia. Mipango itafanywa ili mtaalamu wa teknolojia akutane nawe na kukutathmini katika nyumba yako, shule au mahali pa ajira.
3. Wakati wa mkutano, mtaalamu wa teknolojia atazungumza nawe kuhusu mahitaji yako maalum na malengo ya ajira na anaweza kukuuliza ufanye kazi fulani ili kubaini kiwango chako cha utendaji. Baada ya mkutano, mtaalamu wa teknolojia ataandika ripoti kwa Mshauri wako wa VR akielezea matokeo yake na mapendekezo.
4. Mshauri wako wa VR atashiriki ripoti na wewe na utakuwa na fursa ya kuuliza maswali yoyote ambayo unaweza kuwa nayo kuhusu ripoti. Mara tu wewe na Mshauri wako wa VR mtakapokubaliana kwamba mapendekezo yake ni muhimu kwa kufanikiwa kwa Mpango wako Unaomlenga Mtu Binafsi, mipango itafanywa kununua kifaa au kupanga huduma. Urefu wa muda itachukua kupokea vifaa inategemea aina ya teknolojia, upatikanaji wake na mchakato wa ununuzi.
5. Visaidizi na vifaa vya matakwa ya mteja ambavyo vimeundwa na kutengenezwa mahsusi ili kukufaa vitachukua muda zaidi.
6. DVR itajitahidi kadri iwezekanavyo kukidhi matakwa yako huku ikifuata sera za ununuzi za Serikali ya Jimbo. Ikiwa una bidhaa au muuzaji unayependelea, unapaswa kuhakikisha unamfahamisha mshauri wako.

Katika baadhi ya matukio, unaweza kuhitaji mafunzo ya kujifunza jinsi ya kutumia vifaa hivyo. Wewe na Mshauri wako wa VR mnaweza kupanga jinsi utakavyojifunza kutumia kifaa mara tu unapopokea kifaa hicho. Itakuwa jukumu lako kushirikiana na mafunzo, kufanya mazoezi, na kukamilisha kazi zote ulizopewa.

## Programu ya Mkopo wa Vifaa vya Adaptive (AELP)

Kupitia mpango huu wa unaofadhiliwa dhamana ya jimbo, watu binafsi na biashara wanaweza kupata mikopo ya riba ya chini kutoka $ 250 hadi $ 100,000 ili kuwezesha upatikanaji wa teknolojia ya kusaidia au kuboresha upatikanaji nyumbani au kazini.

Mtu binafsi anaweza kufikia programu ili kupata vitu kama vile:

- Magari au Magari ya Mizigo yenye vidhibiti vya mkono na lifti
- Bafu za Kumiminika
- Vifaa vya usaidizi wa kusikia
- Vifaa vya Kukuza Mawasiliano
- Vifaa vya Mawasiliano kwa Viziwi- TTY
- Kompyuta zinazozungumza kwa sauti
- Lifti za Viti vya Magurudumu na Njia za Rampu
- Mabadiliko ya nyumba
- Vifaa vya burudani (mizunguko ya mkono, viti vya magurudumu ya michezo)

Biashara zinaweza kupata rasilimali ili kupata vitu kama vile:

- Lifti & Eleveta
- Mabadiliko ya Majengo (Viingilio, vyoo, maeneo ya pamoja)
- Mabadiliko ya Maeneo ya Kazi kuwafaa Wafanyakazi
- Magari ya Usafiri yanayofikika kwa urahisi

Mpango huu unasimamiwa na Alpha One.

Kwa taarifa zaidi nenda kwenye: Mpango wa Mkopo wa Vifaa vya Kurekebisha | Alfa ya Kwanza

## Huduma zingine zinazopatikana kutoka kwa Urekebishaji wa Kitaalamu:

### Idara ya Viziwi, Wenye Matatizo ya Kusikia, na Waliopoteza Uwezo wa Kusikia Baadaye (Division for the Deaf, Hard of Hearing, and Late Deafened)

Idara ya Viziwi, Wenye Matatizo ya Kusikia, na Waliopoteza Uwezo wa Kusikia Baadaye ni sehemu ya Idara ya Urekebishaji wa Kitaalamu na hutoa programu ya huduma kwa watu ambao ni viziwi, wenye matatizo ya kusikia, na waliopoteza uwezo wa kusikia baadaye. Mbali na huduma za VR, Idara pia hutoa huduma kama vile: uchapishaji wa Mwongozo wa Rasilimali, Jarida la Maine Lines kwa Viziwi (kijarida), programu zinazoendelea za mafunzo ya vifaa vya mawasiliano na mafunzo mengine kwa mashirika ya jimbo, Utoaji wa taarifa na rufaa, utetezi wa haki, uhamasishaji wa ufikiaji wa huduma, Kadi za Utambulisho wa Viziwi na kuorodhesha wakalimani wa kisheria waliohitimu.

Kwa taarifa zaidi wasiliana au tembelea Tovuti ya DDHHLD

Idara ya Viziwi, Wenye Matatizo ya Kusikia, na Waliopoteza Uwezo wa Kusikia Baadaye
45 Commerce Drive
150 State House Station
Augusta, Maine 04333
Simu ya video 207-470-7668
TTY 207-623-7957

| Kidokezo vya Kusaidia |
| --- |
| Kuna Washauri wa Urekebishaji kwa Idara ya Viziwi, Wenye Matatizo ya Kusikia, na Waliopoteza Uwezo wa Kusikia Baadaye kote katika jimbo |

### Huduma za Maisha ya Kujitegemea

### Mpango wa Huduma za Maisha ya Kujitegemea ni nini?

DVR hupokea fedha kutoka kwa serikali ya kitaifa kwa ajili ya Mpango wa Huduma za Maisha ya Kujitegemea na hupeana kandarasi kwa ajili ya utoaji wa huduma. DVR kwa sasa ina kandarasi na Alpha One, Kituo cha Maine cha Maisha ya Kujitegemea. Mpango wa Huduma za Maisha ya Kujitegemea (ILS) husaidia watu wenye ulemavu mkubwa kuishi kwa kujitegemea zaidi katika nyumba zao na jamii zao. Mpango huu hutoa na kupanga huduma zinazohitajika za IL kulingana na upatikanaji wa fedha. Mpango huo pia ni mpango wa utetezi kwa watu wenye ulemavu na familia zao.
Kwa taarifa zaidi na kutuma maombi kwa Mpango wa ILS, wasiliana na ofisi Alpha One iliyo karibu nawe:

**Alpha One, South Portland**
127 Main Street
South Portland, ME 04106
(207) 767-2159- Sauti
(800) 640-7200 Sauti
(207) 799-8346 Faksi

**Alpha One, Bangor**
11 Bangor Mall Blvd.
Bangor, ME 04401
(207) 941-6553
(800) 300-6016
(207) 941-6410

**Alpha One, Presque Isle**
551 Main St.
Presque Isle, ME 04769
(207) 764-6466 Sauti
(800) 974-6466 Sauti
(207) 764-5396 Faksi

## **Rasilimali**:

## Ninawezaje kufanya uchaguzi mzuri wa kazi?

Kufanya uchaguzi wa kazi kunahusisha kulinganisha uwezo wako, mambo yanayokuvutia, maadili na haiba yako na mahitaji ya ulimwengu halisi wa kazi. Hii ni mchakato unaoendelea unaojumuisha shughuli mbalimbali zilizoundwa kukusaidia kuchagua lengo la kazi. Mshauri wako wa VR anapatikana kukusaidia na mchakato huu.

**Hatua nne za kufanya uchaguzi wa kazi**:

**1.Kujijua mwenyewe:**

Mchakato huanza na uchunguzi wa kina wa wewe mwenyewe. Ni nini kinakuhamasisha? Mambo yanyokuvutia ni yapi? Unafanya vizuri katika nini? Haiba yako ni ipi? Ni masuala gani yanayohusiana na ulemavu yanayoathiri uchaguzi wako wa kazi? Unataka kuishi na kufanya kazi wapi? Hii inaweza kufanywa kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kujitathmini mwenyewe, mahojiano ya kina ya ushauri nasaha na Mshauri wako wa VR, vipimo vya mambo yanayokuvutia au uwezo, uanagenzi wa kujifunza huku ukiwa kazini na vikundi vya kazi.

Kama sehemu ya mchakato huu, mshauri wako anaweza kukuelekeza kwenye Warsha ya Uchunguzi wa Kazi (CEW) ambayo inafanyika katika Kituo cha Kazi na kuendeshwa na wafanyikazi wa DVR. Warsha inashughulikia mambo kama vile matarajio kuhusu kazi, utayari wako kwa kuanza kazi, zana za kutathmini mambo yanayokuvutia na ujuzi wako, zana za kutafuta kazi, na kufanya kazi na Mshauri wako wa VR.

**2.Kukusanya Taarifa za Kitaaluma na Kielimu**:

Kwa kuwa taarifa za kitaalamu na kielimu zinabadilika kila wakati, ni muhimu kukusanya taarifa kuhusu ulimwengu wa kazi na kuamua ni wapi unafaa zaidi. Mshauri wako wa VR anaweza kukusaidia na mchakato huu. Kuna rasilimali kadhaa zinazopatikana kwako kwa taarifa za kazi kupitia Kituo cha Kazi cha Idara ya Kazi ya Maine ya Kazi. Pia kuna shughuli za kitaalamu ambazo zinaweza kusaidia na hatua hii kama vile kutembelea eneo la kazi na kuwatazama watu wanaofanya kazi unayovutiwa nayo au kujaribu kufanya kazi mwenyewe kwa muda mfupi.
Zaidi ya hayo, kuzungumza na waajiri au watu wengine katika sekta inayokuvutia ni njia bora ya kujifunza zaidi kuhusu taaluma unayoifikiria.
Mshauri wako wa VR pia anaweza kuwa na baadhi ya taarifa hii kutokana na mazungumzo na waajiri. Kadri unavyokusanya aina hii ya taarifa zaidi, ndivyo maamuzi yako ya kazi yatakuwa bora zaidi. Katika kuendeleza Mpango wako wa Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira, itakuwa muhimu kushiriki taarifa yoyote uliyokusanya na Mshauri wako wa VR.

Tathmini ya hali- Ikiwa hujui aina ya kazi unayotaka kufanya, au ikiwa Mshauri wako wa VR hana uhakika kuhusu jinsi VR inaweza kukusaidia, mshauri wako anaweza kwanza kupangia uzoefu wa kazi unaolipwa.

Ikiwa maslahi yako ya ajira yanahitaji elimu rasmi na mafunzo, na kuna maswali kadhaa kuhusu usahihi wa mafunzo hayo, mshauri wako anaweza kuandaa tathmini ya elimu ya majaribio. Hapa ndipo utakuwa na fursa ya kujaribu mafunzo machache kama sehemu ya tathmini yako.

**3.Kufanya maamuzi ya kazi na kupata Ulinganifu sahihi:**

Baada ya kupitia mchakato mzuri wa kujitathmini na kukamilisha awamu ya taarifa ya kazi, uko tayari kufanya uamuzi mzuri kuhusu kulinganisha ujuzi, uwezo, maadili na haiba yako na mahitaji ya kazi yako iliyochaguliwa. Wewe na mshauri wako mnaweza kubaini kama aina fulani ya kazi inakufaa, ni kitu ambacho una uwezo wa kukifanya na unafurahia kufanya. Taarifa zilizokusanywa zitatumika katika kazi yoyote zaidi ambazo wewe na VR mtafanya pamoja. Pia, Mshauri wako wa VR anaweza kukusaidia kutathmini mahitaji ya kimwili au ya akili yanayohitajika na marekebisho yanayoweza kufanywa ili kukuwezesha kufanikiwa.

**4.Kupanga mkakati wa hatua:**

Kuandaa Mpango Unaomlenga Mtu Binafsi wa Ajira wa DVR ukiwa na lengo la ajira ambalo linaelezea huduma na misaada utahitaji kufikia lengo lako ni njia moja nzuri ya kupanga hatua. Mshauri wako wa VR anapatikana kusaidia katika kuandaa mpango huu.

# Urekebishaji wa Kitaalamu, Elimu ya baada ya Sekondari,

# Mafunzo na wewe: Mwongozo wa Mtumiaji

**Utangulizi:**
Madhumuni ya sehemu hii ya kijitabu hiki cha maelezo ni kukusaidia kuelewa jinsi Urekebishaji wa Kitaalamu (VR) na Elimu ya Juu zinavyofanya kazi na kuelezea majukumu yote na majukumu na wajibu wa watu wote wanaoshiriki katika mchakato huu.
Taarifa hii inahusu mipango ya mafunzo, ya kielimu na kitaalamu, ambayo inastahiki na kushiriki katika Mpango wa Msaada wa Wanafunzi wa Fedha wa Serikali Kuu. Fomu ya Taarifa ya Msaada wa Fedha itatumika kutambua gharama zako, rasilimali na mchango wa VR kuelekea programu yako.
Ingawa tumefanya juhudi kutambua masuala na wasiwasi muhimu, tunajua utakuwa na maswali. Tafadhali wasiliana na Mshauri wako wa VR wakati hili litatokea. Kumbuka kwamba upangaji nzuri na mawasiliano ya mara kwa mara na ya wazi na wadau wote ndioi ufunguo wa mafanikio katika eneo hili.

**Sheria inasema nini?**
Sheria za serikali kuu na sheria za Maine VR zinasema kwamba ikiwa elimu ya juu inahitajika kwako kufikia lengo la ajira (kazi), VR inaweza kusaidia. Msaada wa VR kwa elimu ya juu hauwezi kutolewa isipokuwa ufanye juhudi kubwa za kupata msaada kutoka kwa vyanzo vingine, ikiwa ni pamoja na misaada ya wanafunzi wa serikali kuu.

**FAFSA:**
Maombi ya Bila Gharama ya Msaada wa Kifedha kwa Wanafunzi kutoka kwa Serikali Kuu (FAFSA) ni fomu iliyokamilishwa na wanafunzi wa sasa na wanaotarajiwa wa chuo (shahada ya kwanza na mhitimu) nchini Marekani ili kubaini uhalali wake wa Msaada wa kifedha wa mwanafunzi. Wanafunzi wote, ambao wanatumia huduma za VR, wanahitaji kujaza fomu hii. FAFSA itabaini ni aina gani ya msaada wa kifedha utapatikana kwako.

**Msaada wa kifedha ni nini?**
Msaada wa kifedha umeundwa kusaidia watu kufikia gharama zao za elimu wakati rasilimali zao hazitoshi. Mwanafunzi anayeamini kwamba rasilimali zake na zile za familia yake hazitoshi kulipia gharama zote za mahudhurio (mafunzo, malazi na chakula, vitabu, usafiri, shughuli za chuo, nk.) anapaswa kutuma maombi ya msaada wa kifedha kupitia Ofisi ya Msaada wa Fedha (FAO) ya taasisi anayopanga kuhudhuria. Aina tatu za msaada zinazopatikana.

- Ruzuku - ni zawadi na ufadhili wa masomo, ambayo haipaswi kulipwa.
- Mikopo - pesa zilizokopwa ili kufidia gharama za shule. Lazima ilipwe, kwa kawaida na riba, kwa kipindi maalum cha muda. Hii kawaida hufanyika baada ya mwanafunzi kuacha shule au kuhitimu.
- Kufanya Kazi huku Ukisoma - ajira, ambayo inawezesha mwanafunzi kupata sehemu ya gharama za shule.

**Mchango Unaotarajiwa wa Familia (Expected Family Contribution) ni Nini**?

Ikiwa hupokei SSI/SSDI au unastahiki kwa 1619b, utatarajiwa kulipa Mchango Unaotarajiwa wa Familia (EFC)

EFC ni nambari ya faharisi ambayo vyuo hutumia kubaini ni kiasi gani cha msaada wa kifedha unastahiki kupokea. EFC yako inahesabiwa kwa kutumia fomula iliyoanzishwa na sheria na taarifa kutoka kwako Maombi ya Bila Gharama ya Msaada wa Kifedha kwa Wanafunzi kutoka kwa Serikali Kuu (FAFSA).

EFC inazingatia mapato ya familia yako yaliyolipiwa kodi na yasiyolipiwa kodi, mali na manufaa (kama vile manufaa ya ukosefu wa ajira au Usalama wa Jamii). Ukubwa wa familia yako na idadi ya wanafamilia ambao watahudhuria chuo katika mwaka huo pia huzingatiwa.

**Je, ninahitajiwa kuchukua mkopo?**

Unahimizwa kuchukua mikopo kwa ajili ya elimu yako lakini hii sio sharti la serikali kuu au jimbo. Hata hivyo, watu wengi wanatambua kuwa mikopo ni sehemu muhimu ya kuhudhuria programu ya elimu ya juu. Chukulia mikopo kama uwekezaji katika maisha yako ya baadaye. Pia, unaweza kuhitaji kufikiria kuchukua mkopo ili kufidia gharama za mahitaji ya msingi ya maisha.

Ikiwa umechelewa kulipa mkopo wa awali wa mwanafunzi, hautaweza kupokea ruzuku yoyote, mikopo ya ziada ya wanafunzi au msaada wa kufanya kazi huku ukisoma. Utahitaji kuonyesha kuwa umefanya jitihada za kuridhisha kurekebisha hali yako ya deni kabla ya VR kuzingatia kubadilisha ruzuku yoyote iliyotolewa. Kama ilivyoelezwa hapo awali, msaada wa VR kwa mafunzo ya elimu ya juu hauwezi kutolewa isipokuwa ufanye juhudi kubwa za kupata msaada kutoka kwa vyanzo vingine.

**Jinsi Urekebishaji wa Kitaalamu unavyoingiana na mchakato wa misaada ya kifedha:**

Mara tu elimu ya sekondari imetambuliwa kama huduma unahitaji kufikia lengo lako la ajira, juhudi iliyopangwa kwa hatua nyingi kati yako, DVR na Ofisi ya Msaada wa Fedha ya shule huanza.

Utaulizwa kukamilisha sehemu ya fomu ya VR ya Msaada wa Fedha. Fomu hii inabadilishwa kati yako, DVR na ofisi ya Msaada wa Fedha ya shule. Inatumika kuthibitisha msaada ya kifedha uliyopewa na FAFSA na shule na kutambua gharama ya mahudhurio.

DVR itatumia taarifa hii kubaini gharama yako halisi ya mahudhurio ikijumuisha gharama zinazohusiana na ulemavu. Mshauri wako wa VR atahesabu msaada ya kifedha uliotolewa na kuondoa gharama za kuhudhuria masomo. Kiasi hiki kinaitwa "Mahitaji Ambayo Hayajatimizwa" (Unmet Need). Mahitaji ambayo hayajatimizwa ndiyo kiasi ambacho VR itachangia katika gharama ya elimu yako. Kwa wanafunzi wanaopokea SSI/SSDI, mahitaji yao yote ambayo hayajatimizwa yanapaswa kugharamiwa na DVR.

**Ni gharama gani za kielimu zinazochukuliwa kuwa zinazohusiana na ulemavu?**

Mwanafunzi mwenye ulemavu mara nyingi hukabiliwa na gharama za ziada ambazo hazitolewi na wanafunzi wengine. Mifano ya gharama hizi ni pamoja na:

- Ununuzi na matengenezo ya vifaa vinavyohusiana na ulemavu
- Gharama ya huduma kwa matumizi ya kibinafsi au masomo kama vile wasomaji, au wasaidizi wa huduma za kibinafsi
- Usafiri unaohitajika kufuata mpango wa kitaaluma, ikiwa usafiri wa kawaida haupatikani
- Gharama za matibabu zinazohusiana moja kwa moja na ulemavu wa mtu binafsi ambazo hazigharamiwi na bima
- Chakula na gharama za matibabu za mbwa wa mwongozo
- Betri za vifaa vya kusikia na Vifaa vya Mawasiliano kwa Viziwi
- Gharama za kuajiri na kufundisha wasomaji au wasaidizi wa huduma ya kibinafsi

Mara nyingi, kuondoka nyumbani kunahitaji ununuzi wa vifaa vipya au vya ziada ambavyo vitamruhusu mwanafunzi kujitegemea shuleni. Baadhi ya vifaa na huduma za msaada zinaweza kupatikana katika taasisi za elimu ya juu. Wewe na Mshauri wako wa VR mnapaswa kuwasiliana na Mratibu wa 504 au Ofisi ya Huduma za Usaidizi wa Ulemavu katika taasisi hiyo ili kuona kile kinachopatikana hapo.

**Majukumu yangu ni yapi?**

Kuhudhuria elimu ya juu huja na majukumu mbalimbali. Hizi ni pamoja na:

- Kutuma maombi na kukamilisha fomu ya taarifa ya Msaada wa Fedha kwa wakati unaofaa
- Kuchunguza rasilimali zingine za ufadhili ambazo zinaweza kusaidia kugharamia baadhi ya gharama zingine za elimu ya juu. Mifano ya rasilimali hizi ni pamoja na Mpango wa Kufikia Msaada wa Kujitegemea (PASS-Plan for Achieving Self Support), Ticket to Work, ASPIRE, VA na Kituo cha Maendeleo ya Kazi
- Kudumisha angalau masaa sita ya alama za muamana kwa muhula ili kuonyesha maendeleo ya kitaaluma
- Kubaki katika msimamo mzuri wa kitaaluma na taasisi unaposomea
- Fanya mazoea ya kumpa mshauri wako nakala ya alama zako mara kwa mara.
- Kutana na idara ya huduma za ulemavu ili kufanya mipango ya malazi yoyote unayohitaji
- Utahitajika kumjulisha Mshauri wako wa VR kuhusu mabadiliko yoyote katika hali yako, ama vile kubadilika kutoka masomo ya muda wote hadi masomo ya muda mfupi, na matatizo yoyote unayokutana nayo katika taasisi

**Mahali pa Kupata ya Taarifa za Ziada:**

Mshauri wako wa VR na FAO wanapaswa kuwa na uwezo wa kujibu maswali uliyo nayo. Hapa ni baadhi ya mahali kupata taarifa zaidi.

1.Tovuti ya Msaada wa Wanafunzi wa Serikali Kuu ina rasilimali kadhaa na inachapisha kijitabu cha maelekezo kinachoitwa "Kufadhili Elimu Baada ya Shule ya Upili" ambacho kinapatikana katika https://files.eric.ed.gov/fulltext/ED490979.pdf

2. Mamlaka ya Fedha ya Maine (FAME) ni mpango ambao unaweza kuwa rasilimali kwa wanafunzi ambao wanataka kuendeleza elimu yao. Kwa taarifa zaidi:

Mamlaka ya Fedha ya Maine (FAME)

5 Community Drive, P.O. Box 949
Augusta, ME 04332-0949
SIMU: (207) 623-3263 au 1-800-228-3734

- TTY: (207) 626-2717

FAKSI: (207) 623-0095

http://www.famemaine.com/

3. Mpango wa Msaada wa Mteja (CAP) ni mpango wa utetezi unaofadhiliwa na serikali kuu ambao unaweza kutoa taarifa na, ikiwa inahitajika, uwakilishi kwa wateja/waombaji wa VR. Kwa taarifa zaidi angalia ukurasa wa 12 wa kijitabu hiki maelekezo

Msaada wa kifedha unategemea ushirikiano kati ya mwanafunzi, wazazi, taasisi za masomo baada ya sekondari, serikali kuu na mashirika kama vile VR. Mchakato wa msaada ya kifedha unaweza kuwa changamani na unaochukua muda mrefu. Inahitaji uratibu, ushirikiano na mawasiliano kati ya FAO, Mshauri wa VR na wewe.

## Ofisi za Idara ya Urekebishaji wa Kitaalamu

Augusta
45 Commerce Drive
Augusta, ME 04330-0073
624-5120 au 1-800-760-1573
TTY Tafadhali tumia Mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
287-6249 (Faksi)

Bangor
45 Oak Street, Suite 1
Bangor, ME 04401-6589
561-4000 au 1-888-545-8811
TTY Tafadhali tumia Mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
561-4027 (Faksi)

Hinckley
23 Stanley Rd
Hinckley, ME 04944
474-4958 au 1-800-760-1572
TTY tafadhali tumia mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
453-2501 (Faksi)

Houlton
11 High St.
Houlton, ME 04730-2421
532-5019 au 1-800-432-7338
TTY Tafadhali tumia Mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
532-7995 (Faksi)

Lewiston
5 Mollison Way
Lewiston, ME 04240-5805
753-9000 au 1-800-741-2991
TTY Tafadhali tumia Mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
753-9051 (Faksi)

Machias
53 Prescott Drive, Suite 2
Machias, ME 04654-9751
255-1926 au 1-800-770-7774
TTY Tafadhali tumia Mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
255-1926 (Faksi)

Portland
151 Jetport Blvd.
Portland, ME 04102
822-3300 au 1-877-594-5627
TTY Tafadhali tumia Mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
775-7870 (Faksi)

Presque Isle
66 Spruce Street, Suite 3
Presque Isle, ME 04769
760-6300 au 1-800-635-0357
TTY Tafadhali tumia Mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
760-6316 (Faksi)

Ofisi ya Utawala
45 Commerce Drive
Augusta, ME 04330-0073
207-623-6799
TTY tafadhali tumia Mtambo wa kupokea na kurushia habari 711
207-287-5292 (Faksi)